

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF AGRICULTURE



TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES
AUTHORITY (TPHPA)



**TAMKO LA MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUTILIFU TANZANIA
(TPHPA)**

**KUTANGAZA ENEO LA NYANDA ZA JUU KUSINI KUWA NI ENEO
HURU LA UGONJWA WA VIRUSI VYA MAHINDI (UVIMA)**


Ugonjwa wa Virusi vya Mahindi (UVIMA) ulitangzwa kuingia nchini kwa mara kwanza Mwezi August 2012, katika maeneo ya Manyara, Arusha na Moshi na baadae ukaenea maeneo ya kanda ya ziwa Mikoa ya Mwanza, Musoma, Simiyu na Kagera. Ugonjwa huu hutokea tu pale yanapokuwepo mashambulizi ya pamoja kati ya kirusi aina ya MCMV na kirusi chochote kutoka kundi la Potyviridae kama vile SCMV, MDMV, WSMVn.k

Katika kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu, Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viutilifu Tanzania (TPHPA) imeendelea kuchukua hatua zifuatazo kwa mujibu wa kanuni ya 106 ya Kanuni za Afya ya Mimea za 2023;

1. Kufanya aua (survey) kila mara maeneo yote ya uzalishaji mahindi nchini ili kutambua hali halisi ya ueneaji wa ugonjwa huu, na kuchukua hatua za kuutokomeza;
2. Kuchukua sampuli na kupima virusi vya MLN kwenye mbegu zote za mahindi zinazoingia nchini kutoka nchi zinazojulikana zina ugonjwa huu;
3. Kuelimisha wakulima kuitia machapisho, warsha na vipindi mbalimbali vya redio. Zaidi ya vipeperushi elfu arobaini (40,000) na miongozo zaidi ya elfu ishirini (20,000) ya kudhibiti ugonjwa huu ilichapishwa na kugawiwa kwa wakulima na maafisa ugani katika mikoa yote;
4. Kukagua mashamba ya mbegu wakati wa uzalishaji na kuyathibitisha (certify) kabla ya kuanza kusambaza na kuuza mbegu;

5. Matokeo ya aua yaliyofanyika kwa mujibu wa aya ya (1) hapo juu yamethibitisha kuwa, sampuli zote zilizochukuliwa na kupimwa katika maeneo ya nyanda za juu kusini hazijawahi kugundulika na ugonjwa wa UVIMA;
6. Ikumbukwe kabla ya kuwepo kwa Sheria ya Afya ya Mimea (Sura ya 133) na Kanuni zake za 2023, Wizara ya Kilimo ilitunga na kusimamia kanuni ndogo za Afya ya Mimea zilizotangazwa katika gazeti la serikali la tarehe 21/06/2013 kwa notisi Na.195 Kanuni hizi pamoja na kuweka wajibu kwa mkulima kutoa taarifa haraka punde anapoona ugonjwa huu shambani kwake pia zinazuia usafirishaji wa mbegu kutoka maeneo yaliyo athirika na ugonjwa;

Kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha Sheria ya Afya ya Mimea (Sura ya 133), kikisomwa pamoja na kanuni ya 106 ya Kanuni za Afya ya Mimea za Mwaka 2023, na kwa kuzingatia hatua za udhibiti kama zilivyoainishwa hapo juu, NATANGAZA eneo la Nyanda za Juu Kusini linalojuimisha mikoa ya Katavi, Rukwa, Njombe, Songwe, Mbeya, Iringa Ruvuma pamoja na Mikoa ya jirani kuwa ni eneo huru la ugonjwa wa UVIMA. Aidha, nasisitiza kila mwananchi kuendelea kuwa makini ili kudhibiti ueneaji wa ugonjwa huu katika maeneo mengine ya Tanzania.



Joseph C. Ndunguru
MKURUGENZI MKUU